**Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.**

Budget Documents Government Budget Speeches

1998-06-11

# Hotuba ya Waziri wa Fedha Mh. Daniel Yona akiwasilisha mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 1998 - 1999

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wizara ya Fedha

https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/668

*Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA MHESHIMIWA DANIEL N. YONA (MB.) KATIKA BUNGE TAREHE 11 JUNI, 1998 AKIWASILISHA MAPENDEKEZO YA SERIKALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA 1998/99

1998
KIMEPIGWA CHAPA NA MPIGACHAPA WA SERIKALI
DAR ES SALAAM—TANZANIA

# HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA MHESHIMIWA DANIEL N. YONA (MB.) KATIKA BUNGE TAREHE 11 JUNI, 1998 AKIWASILISHA MAPENDEKEZO YA SERIKALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA 1998/99

## UTANGULIZI:

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likae kama Kamati ili liweze kujadili na hatimaye kuidhinisha mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi katika mwaka wa fedha wa 1998/99. Pamoja na hotuba hii vipo vitabu viwili. Kitabu cha kwanza kinahusu makisio ya mapato ya Serikali kwa mwaka ujao na kitabu cha pili ni cha makisio ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Aidha, upo pia mswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 1998/99. Bunge lako Tukufu linaombwa kujadili kwa kina yaliyomo katika,

hotuba, vitabu pamoja na miswada kwa lengo la kuidhinisha bajeti ya Serikali ya mwaka ujao.

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru wote waliohusika katika kutayarisha bajeti hii. Kwanza, natoa shukrani zangu za dhati kwa Wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha, Tume ya Mipango, Wizara mbalimbali, Mikoa na Halmashauri zake, Taasisi za kitaifa na vikundi mbalimbali vilivyochangia katika matayarisho ya bajeti ya Serikali. Nachukua nafasi hii pia kuishukuru Wizara ya Sheria kwa kutayarisha miswada mbalimbali ambayo ni sehemu ya bajeti hii. Aidha, nazipongeza Kamati za Uchumi na Fedha na Ulinzi na Usalama za Bunge lako Tukufu kwa kazi nzuri zilizoifanya ya kupitia makadirio ya bajeti kwa vyombo mbalimbali vya Serikali na kutoa ushauri wa kuboresha makisio hayo. Ushauri wao umezingatiwa vizuri katika kuboresha na kukamilisha matayarisho ya bajeti hii.

3. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka huu wa fedha tumeshuhudia matukio mengi yanayotugusa kama wabunge. Kwa upande wa Bunge lako Tukufu, baadhi ya Wabunge ambao tulikuwa nao katika kikao kama hiki mwaka jana hatunao tena kutokana na sababu mbali mbali. Wabunge hao ni Mheshimiwa Tuntemeke Sanga Nnungi aliyekuwa Mbunge wa Makete, Mheshimiwa Joseph Monko aliyekuwa Mbunge wa Singida Kaskazini, Mheshimiwa Mwita Hassan Khatib aliyekuwa Mbunge wa Mikunguni na Mheshimiwa Mary Kabigi aliyekuwa Mbunge, Viti Maalum Wanawake, ambao wote ni marehemu. Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi. Mbali na Wabunge hao, pia wapo Wabunge ambao kutokana na matatizo mbalimbali hawapo hapa Bungeni pamoja nasi leo. Wabunge hao ni Mheshimiwa Makongoro Charles Nyerere aliyekuwa Mbunge wa Arusha, Mheshimiwa Sebastian Nzebayo Kanga aliyekuwa Mbunge wa Kahama, Mheshimiwa Paulo Maholo aliyekuwa Mbunge wa Kishapu, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai aliyekuwa

Mbunge wa Ubungo na Mheshimiwa Sebastian Rweikiza Kinyondo aliyekuwa Mbunge wa Bukoba. Hawa nao tunawashukuru kwa michango yao na tunawatakia kheri na fanaka katika kujenga Taifa kokote waliko. Aidha, katika kipindi hicho Bunge lako Tukufu limepata Wabunge wapya. Wabunge hao ni Mheshimiwa Besen Hassy Kitine Mbunge wa Makete, Mheshimiwa Felix Christopher Mrema Mbunge wa Arusha, Mheshimiwa Raphael Nkuli Mlolwa Mbunge wa Kahama, Mheshimiwa Alute Joram Sima Mbunge wa Singida Kaskazini na Mheshimiwa Juma Duni Haji, Mbunge wa Mkunazini. Naomba niwapongeze Wabunge hawa wapya na ni matumaini yangu kuwa tutashirikiana katika kusimamia maendeleo ya uchumi na jamii ya nchi yetu.

4. Mheshimiwa Spika, Watanzania katika mwaka huu wa fedha wameshuhudia madhara mengi na ya uzito mkubwa ambayo yameathiri uchumi wetu. Waziri wa Nchi Mipango, Mheshimiwa Nasoro Malocho (MB.), katika hotuba yake leo asubuhi

alielezea hali ya uchumi ilivyokuwa katika mwaka huu wa fedha 1997/98. Hivyo nisingependa kurudia kwa kirefu maelezo ambayo yamekwishatolewa.

5. Mheshimiwa Spika, ingawa uchumi wetu unaonyesha kukua, kiwango cha ukuaji wake cha wastani wa asilimia 3.5 hakiridhishi ukilinganisha na mahitaji ya wananchi ambao huongezeka kwa wastani wa asilimia 2.8 kila mwaka. Kwa maana hii, ongezeko halisi la pato kwa kila Mtanzania ni chini ya wastani wa asilimia moja kwa mwaka. Ukuaji wa pato halisi la kila Mtanzania kwa kiwango hiki halituhakikishii maendeleo tunayotaka. Ni wajibu wa Watanzania wote kuelewa tatizo hili na kushirikiana na Serikali kulitafutia ufumbuzi wa haraka na wa kudumu.

**TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA SERA ZA BAJETI YA MWAKA 1997/98:**

6. Mheshimiwa Spika, naomba sasa nielezee tathmini ya utekelezaji wa Sera za bajeti ya mwaka 1997/98.

7. Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba, katika mwaka wa fedha 1997/98, Serikali iliweka sera na mikakati mbalimbali iliyolenga katika kuimarisha uchumi, kuongeza mapato ya ndani na kudhibiti matumizi. Mikakati hiyo iliegemea katika misingi ifuatayo:-

i) Kukuza uchumi kwa asilimia 4.5;

ii) Kupunguza mfumuko wa bei kutoka wastani wa asilimia 15 mwaka 1996/97 hadi asilimia 10 kwa mwaka 1997/98;

iii) Kupunguza nakisi katika urari wa kawaida wa malipo na nchi za nje na;

iv) Serikali kujitegemea zaidi katika Bajeti yake.

8. Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia misingi hiyo ya kiuchumi, malengo ya Bajeti ya mwaka 1997/98 ilikuwa kama ifuatavyo:

i) Kukusanya ya Shs. 695,300 milioni

ikiwa ni mapato ya ndani na Shs. 302,100 milioni ikiwa ni mapato ya nje.

ii) kutumia jumla ya Shs. 975,639 milioni. Kati ya hizo Shs. 666,843 milioni ni matumizi ya kawaida na Shs. 308,796 milioni ni matumizi ya maendeleo.

iii) Kuwa na ziada katika matumizi ya kawaida ya Shs. 76,612 milioni (bila kujumuisha malipo ya madeni yaliyopevuka);

iv) Kupunguza limbikizo la deni la Serikali katika mabenki kwa Shs. 59,595 milioni; na

v) Kupunguza kiwango cha malimbikizo ya madeni ya Wizara, Idara na Mikoa pamoja na kuepuka madeni mapya.

**Sera za Mapato:**

9. Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia misingi ya bajeti iliyoelezwa hapo juu, Sera za Mapato katika mwaka 1997/98 zilikuwa kama ifuatavyo:-

i) Kuimarisha makusanyo ya mapato kwa kurekebisha sera za kodi ili kulinda viwanda vyetu na kuendeleza uchumi kwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji, uzalishaji, na utoaji huduma;

ii) Kuondoa au kurekebisha baadhi ya kodi zilizokuwa kero kwa wananchi;

iii) Kuhakikisha kuwa Sekta mbalimbali zinachangia katika mapato ya Serikali kwa kuweka viwango vya kodi katika huduma ambazo hazitozwi kodi; na

iv) Kutayarisha mazingira ya kuanzisha kodi ya ongezeko la thamani (VAT).

10. Mheshimiwa Spika, Serikali imetekeleza karibu sera zote za mapato katika mwaka wa fedha 1997/98. Hata hivyo, utekelezaji wa sera hizo uliathiriwa na kuendelea kuwapo kwa ukame wa muda mrefu, ukwepaji kodi, kuendelea kwa misamaha fulani fulani ya kodi, uharibifu wa njia za usafirishaji kutokana na madhara ya hali ya hewa ya EL-NINO na upungufu wa uagizaji kutoka nje.

11. Mheshimiwa Spika, ukame uliokuwapo katika nusu ya kwanza ya mwaka huu wa fedha ulisababisha mazao mengi ya kilimo kukauka. Aidha, ukosefu wa maji pia ulipunguza nishati hasa viwandani na hivyo kuathiri uzalishaji. Mabadiliko ya hali ya hewa ya EL-NINO kuanzia mwishoni mwa mwaka 1997 yameleta mvua nyingi ambayo imesababisha maafa sehemu nyingi nchini. Kutokana na mvua hizo, njia za

usafirishaji karibu zote zimeathirika. Hali hii imesababisha bidhaa nyingi kukwama viwandani na bandarini na hivyo kuathiri mapato ya Serikali.

12. Tatizo jingine ambalo Serikali imekuwa ikilishughulikia ni ukwepaji wa kodi. Pamoja na juhudi za Serikali za kupambana nalo bado tatizo hili lipo. Bidhaa za nguo, mafuta ya kupikia, sabuni, viatu, matairi, betri za magari, Radio na sasa hata mafuta ya petroli zinaongoza katika kuendelea kukwepa kodi. Aidha, kuna baadhi ya misamaha ya kodi ambayo imekuwa inaendelea na hivyo kusababisha mapato ya Serikali kupungua. Misamaha hiyo itabidi tuiangalie upya kwa lengo la kuirekebisha.

**Mikopo na Misaada ya Nje:**

13. Mheshimiwa Spika, Serikali katika bajeti ya mwaka 1997/98 iliweka sera za mikopo na misaada ya nje kwa mwaka huo. Sera hizo ni pamoja na kuendelea na mipango ya kurekebisha uchumi inayodhaminiwa na Shirika la Fedha la Kimataifa

(IMF) na Benki ya Dunia kwa niaba ya Wahisani wengine. Aidha, Serikali iliendelea kujadiliana na wahisani mbalimbali ili kutusaidia huku ikizingatiwa kuwa misaada hiyo siyo ya kutegemewa sana katika kutuletea maendeleo. Hadi sasa Serikali inaendelea kutekeleza mpango wa IMF wa "Enhanced Structural Adjustment Facility" (ESAF) na mpango wa Benki ya Dunia wa "Structural Adjustment Credit" (SAC). Mipango hii inatusaidia kupata mikopo nafuu ya fedha za kigeni na kuchangia katika bajeti ya Serikali. Mbali na mikopo kutoka katika vyombo hivi, misaada mingine kutoka kwa Wahisani mbalimbali imesadia sana bajeti ya Serikali. Kwa niaba ya Serikali, nachukua fursa hii kuwashukuru Wahisani wote kwa misaada yao waliyotupa na wanayoendelea kutupa.

**Mikopo ya Ndani:**

14. Mheshimiwa Spika, kuhusu mikopo ya ndani ambayo inajumuisha vyombo vya mabenki na visivyo vya mabenki, Serikali iliazimia ifuatavyo:

(a) Kutokopa kabisa kutoka Mabenki na badala yake kupunguza madeni ya Serikali kwa vyombo hivyo kwa kiasi cha Shs. 59,695 milioni;

(b) Kutokopa kutoka vyombo visivyokuwa vya mabenki hasa Dhamana za Hazina (Treasury Bills) isipokuwa kwa ajili ya kulipia Dhamana zinazopevuka;

Mwenendo unaonyesha kuwa, hadi mwishoni mwa mwezi Aprili, 1998, Serikali iliweza kupunguza limbikizo la madeni yake katika mabenki kwa kiasi cha Shs. 48,199.9 milioni. Aidha, hadi Aprili, 1998 Serikali ilikuwa imekopa kutoka vyombo visivyo vya mabenki Shs. 18,465.8 milioni kwa utaratibu wa dhamana.

**Matumizi:**

15. Mheshimiwa Spika, sera za matumizi zinazotekelezwa katika mwaka 1997/98 ni pamoja na kuendelea na utaratibu wa matumizi kulingana na

mapato (Cash Budgeting), kutoa upendeleo maalum wa mgao wa fedha kwenye sekta ya huduma za jamii, kupunguza malimbikizo ya madeni ya ndani na kupunguza sana miradi ya maendeleo ili kubakiza michache inayoweza kugharamiwa kikamilifu. Serikali iliweza kutekeleza sera hizi kama ilivyoazimia. Utaratibu wa "Cash Budgeting" ulitekelezwa na kwa mwaka huu ulikuwa na nafuu zaidi kuliko ilivyokuwa mwaka 1996/97.

16. Pamoja na "Cash Budgeting", baadhi ya mafungu yamepata mgao wa kila mwezi kulingana na bajeti zao. Mafungu hayo ni ya bajeti za mikoa na halmashauri, bajeti ya Ngome na JKT, deni la Taifa, Vyuo Vikuu na madawa ya hospitali. Kwa upande wa ulipaji madeni ya ndani, Serikali hadi mwezi Aprili ilikuwa imelipa jumla ya shs. 20,052.6 milioni. Madeni hayo ni ya TANESCO, Wazabuni, Duty Draw Back, posho za Polisi, ruzuku ya mbolea na malimbikizo ya madeni yatokanayo na nyongeza za mishahara kwa mashirika ya umma.

## MWENENDO NA MWELEKEO WA BAJETI YA MWAKA 1997/98

17. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo kuhusu sera za bajeti kwa mwaka 1997/98, naomba sasa nieleze mwenendo wa bajeti ya mwaka huu wa fedha. Kwa upande wa mapato, hadi kufikia mwezi Aprili, 1998 jumla ya Shs. 512,709.2 milioni zilikuwa zimekusanywa. Kiasi hiki kinazidi makusanyo ya mwaka 1996/97 kwa kipindi kama hicho kwa Shs. 44,181.2 milioni sawa na asilimia 9. Mwenendo huo mzuri unatokana na mikakati mbalimbali iliyofanywa na Serikali ijapokuwa nchi yetu ilikabiliwa na matatizo mbalimbali yaliyoathiri sekta zetu za uzalishaji kama nilivyoeleza wakati nikizungumzia sera za mapato hapo juu. Kutokana na mwenendo huu wa mapato, mwelekeo wa makusanyo ya mapato hadi kufikia mwisho wa Juni, 1998 ni kupata jumla ya shs. 627,500 milioni.

18. Mheshimiwa Spika, mwenendo wa makusanyo ya mapato yatokanayo na misaada na mikopo kutoka nje kwa kipindi cha Julai, 1997 hadi Aprili, 1998 unaonyesha kuwa jumla ya Shs. 214,864 milioni zilipatikana ikiwa ni asilimia 71 ya makisio ya Sh. 302,100 milioni. Matarajio hadi mwisho wa Juni 1998 ni kupata jumla ya shs. 243,400 milioni. Kwa upande wa mikopo ya ndani hadi Aprili, 1998 Serikali ilikopa jumla ya Shs. 35,759.9 milioni kutoka kwenye vyombo visivyo vya mabenki. Kati ya hizo, Shs. 18,465.8 milioni zimekopwa kwa utaratibu wa Dhamana za Hazina (Treasury Bills). Vile vile, Serikali imelazimika kukopa kwa utaratibu wa "Promissory Notes" (PN) jumla ya shs. 17,294.1 milioni ili kukidhi mahitaji ya vyombo vya usafiri vya ulinzi na usalama hasa wakati ule wa matatizo ya jirani zetu wa Burundi. Hata hivyo, siyo nia ya Serikali kuendelea tena kukopa kwa utaratibu huu. Kwa upande wa mikopo kutoka mabenki, Serikali iliweza kupunguza limbikizo la madeni yake katika vyombo hivyo kwa kiasi cha Shs. 48,199.9 milioni hadi mwisho wa mwezi Aprili, 1998.

Kwa maana hii, mikopo ya ndani ambayo inajumuisha vianzio vya mabenki na visivyo vya mabenki ilionyesha kupungua kwa Shs. 12,440 milioni hadi Aprili 1998. Serikali inalenga kumaliza mwaka huu wa fedha bila kuendelea kukopa mikopo ya aina hii.

19. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi, hadi kufikia mwisho wa mwezi Aprili 1998, Serikali ilikuwa imetumia jumla ya Shs. 691,670 milioni ikiwa ni asilimia 71 ya matumizi yaliyokadiriwa. Kati ya fedha hizo, Shs. 537,837.2 milioni ni za matumizi ya kawaida na Shs. 153,822.8 milioni ni za matumizi ya maendeleo. Matumizi ya kawaida ni sawa na asilimia 81 ya makadirio, wakati yale ya maendeleo ni asilimia 50 ya makadirio ya bajeti. Kutokana na mwenendo huu, mwelekeo wa matumizi hadi mwisho wa Juni, 1998 ni kufikia jumla ya Shs. 866,951 milioni ikiwa ni upungufu wa asilimia 11 ya makadirio ya bajeti. Kati ya matumizi hayo, Shs. 711,851 milioni ni za matumizi ya kawaida na Shs. 155,100 milioni ni za matumizi ya maendeleo.

**Sekta ya Fedha:**

20. Mheshimiwa Spika, baada ya kuelezea tathmini ya bajeti, sasa naomba nielezee kwa muhtasari tathmini ya sekta ya fedha. Ili kuleta chachu ya maendeleo katika nchi yoyote duniani ikiwa ni pamoja na Tanzania, sekta ya fedha ni budi iwe imara hasa katika kudhibiti ujazi wa fedha (money supply) na mfumuko wa bei (inflation). Benki Kuu ya Tanzania kwa niaba ya Serikali imeendelea kudhibiti mfumuko wa bei na ujazi wa fedha. Mfumuko wa bei hadi Aprili, 1998 ulifikia asilimia 13.5 na inategemewa kufikia asilimia 10 hapo Juni 30, 1998. Aidha, kwa kudhibiti Bajeti ya Serikali na kutokopa kutoka mabenki kumesaidia sana katika kuweza kufikia lengo la kudhibiti ujazi wa fedha na kupunguza mfumuko wa bei. Katika mwaka 1997/98, sekta ya fedha iliendelea kufanyiwa marekebisho. Itakumbukwa kuwa tarehe 1 Oktoba, 1997 iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) iligawanywa kwa kuunda Benki mbili yaani NBC (1997) Limited na National Microfinance Bank (NMB) Ltd. Aidha, madeni yote sugu na ziada ya mali

isiyohamishika (non core assets) ilikabidhiwa "NBC Holding Corporation" ili kuziuza na kuwekeza fedha hizo katika Benki hizo, tayari kwa ubinafsishaji. Hatua zote hizi zinalenga katika kuwa na sekta imara ya fedha ambayo itajitegemea.

**Sekta ya Nje:**

21. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 1997/98, hali ya maendeleo ya sekta ya nje haikuwa ya kuridhisha sana. Mauzo ya bidhaa nje yanategemewa kupungua kutoka dola za kimarekani 794 milioni katika mwaka 1996/97 hadi kufikia dola za kimarekani 678 milioni mwaka 1997/98, ikiwa ni upungufu wa asilimia 15. Bidhaa asilia (traditional exports) zimepungua kutoka dola za kimarekani 410 milioni hadi dola za kimarekani 337 milioni sawa na asilimia 18. Mauzo ya bidhaa zisizoasilia (non traditional exports) nayo yalipungua kwa asilimia 11 kutoka dola za kimarekani 384 milioni katika mwaka 1996/97 hadi dola za kimarekani 341 katika mwaka 1997/98. Pamoja na kwamba bei ya mazao yote asilia imeongezeka

isipokuwa zao la tumbaku, ongezeko hilo halikuwafaidisha zaidi wauzaji wetu. Hii inatokana na ukweli kwamba ongezeko hilo la bei linatokana na kupungua kwa wingi wa bidhaa hizo kwenye soko la dunia. Uuzaji wa madini nje ya nchi umeonyesha mafanikio makubwa. Mauzo ya bidhaa hii yameongezeka kutoka dola za kimarekani 58 milioni mwaka 1996/97 hadi Dola za kimarekani 112 milioni mwaka 1997/98 sawa na ongezeko la asilimia 93.

22. Kwa upande wa uagizaji bidhaa nje, mwenendo unaonyesha ongezeko kutoka Dola za kimarekani 1,388 milioni mwaka 1996/97 hadi Dola za kimarekani 1,508 milioni mwaka 1997/98, ikiwa ni ongezeko la karibu asilimia 9.
Kuongezeka kwa uagizaji bidhaa nje kulijitokeza zaidi kwa bidhaa za mitambo, malighafi za viwandani na vyakula. Aidha, kulikuwa na upungufu katika uagizaji wa bidhaa za mafuta ya petroli. Mwenendo huo unaonyesha kuwa bado kuna pengo kati ya bidhaa na huduma zetu tulizouza na zile tulizoziagiza kutoka nje ya nchi.

**Mashirika ya Umma:**

23. Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali katika utekelezaji wa Sera ya Mashirika ya Umma ni kuhakikisha kuwa yanaondokana na utegemezi kwa Serikali na kujiendesha kwa ufanisi. Katika kutekeleza azma hii, Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC), Tume ya Mipango na Urekebishaji Mashirika ya Umma na Wizara mama (Sector Ministries) imeendelea na utaratibu wa kurekebisha mashirika hayo kwa nia ya kuyauza, kuingia ubia na wawekezaji wa ndani na nje na pale yanapoonekana kutorekebishika au kutouzika kuyafilisi. Hadi kufikia Mei, 1998, kati ya Mashirika 398 yaliyopelekwa PSRC, 201 yamekwishabinafsishwa.

24. Mheshimiwa Spika, kama inavyofahamika, Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) limeshaanza kazi rasmi tarehe 15 April, 1998 kwa kuuza hisa za

Kampuni ya Tanzania Oxygen Limited (TOL). Aidha, Kampuni ya Bia Tanzania (TBL) imeanza kuuza asilimia 10 ya hisa za Serikali kwa wananchi kupitia Soko hilo kuanzia mwezi Mei, 1998. Ni matumaini yangu kuwa Waheshimiwa Wabunge, kama wananchi wengine, sasa hivi wananunua hisa hizo tunazouza kwenye soko la Hisa la Dar es Salaam. Makampuni mengine ya Sigara (TCC), ya kusambaza mafuta ya BP na AGIP na Viwanda vya Tanga Cement Company Ltd na Tanzania Portland Cement (Wazo) Ltd wameshaanza maandalizi ya kuuza sehemu ya hisa za Serikali katika Soko la Hisa.

25. Mheshimiwa Spika, kwa vile lengo kubwa la Serikali ni kuona kuwa mashirika makubwa na muhimu katika uchumi wa Tanzania yanajiendesha vizuri, Serikali imeshaanza utaratibu wa kuyarekebisha na hatimaye kubinafsisha mashirika ya huduma (public utilities) kama vile Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka (DAWASA),

Mamlaka ya Bandari Tanzania (THA), Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL) na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

**Sekta Binafsi:**

26. Mheshimiwa Spika, kufuatia sera ya ubinafsishaji inayoendelea hivi sasa, sekta binafsi imeshachukua nafasi kubwa katika maendeleo ya uchumi wetu. Kama nilivyoeleza, hivi sasa zaidi ya mashirika 201 kati ya 398 yaliyokuwa ya umma yameshaingia katika miliki ya Sekta binafsi. Aidha, kwa Serikali kuruhusu biashara huria na kwa kuboresha vivutio kwa wawekezaji wa ndani na nje chini ya utaratibu wa Kituo cha Uwekezaji "Tanzania Investment Centre" (TIC), sekta hii imeanza kuchangia asilimia kubwa zaidi katika pato la Taifa. Kuanzishwa kwa Soko la Hisa la Dar es Salaam, kumetoa nafasi kubwa kwa wananchi hasa wenye vipato vidogo kuweza kununua na kumiliki hisa za makampuni ya kibiashara kama Serikali ilivyodhamiria. Ni nia ya Serikali kuruhusu uuzaji wa hisa zaidi pale makampuni yaliyokwisha

binafsishwa na ambayo Serikali bado inashikilia hisa yatakapo kuwa na hali nzuri ya kifedha na uendeshaji (good performance track record).

**Madeni ya ndani:**

27. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 1997/98, Serikali iliendelea kutekeleza mpango wake wa kupunguza mzigo wake wa madeni ya ndani na nje ya nchi. Deni la ndani la Taifa lilikadiriwa kufikia shilingi 859.6 bilioni katika mwaka 1997/98. Njia mbali mbali zilizotumika katika kupunguza madeni ya ndani ilikuwa ni pamoja na kubadilisha madeni yaliyo na viwango vikubwa vya riba kuwa madeni mapya yenye viwango vidogo vya riba (Debt substitution). Madeni yaliyohusika ni yale ambayo Serikali ilikopa kutoka Benki Kuu kwa kubadilisha madeni ya muda mfupi (direct advances) kuwa ya muda mrefu (longterm debt), na Serikali ilitoa dhamana za muda mrefu (long term stocks).

**Madeni ya Nje:**

28. Madeni ya nje sasa yanakadiriwa kuwa Dola za Kimarekani 7.9 bilioni. Kwa upande wa madeni haya, Serikali iliendeleza jitihada zake za kuyadhibiti madeni kwa nia ya kuyapunguza au kusitisha ukuaji wake. Hii ilijumuisha:

i) Mpango wa ulipaji wa madeni chini ya utaratibu wa unafuu wa madeni wa nchi wanachama wa Paris Club;

ii) Mpango wa ulipaji wa madeni tunayodaiwa na Taasisi za Kimataifa kama vile Benki ya Dunia au Shirika la Fedha la Kimataifa na taasisi nyingine;

iii) Mpango wa kuyanunua malimbikizo ya madeni binafsi ya kibiashara chini ya utaratibu wa "Debt Buy Back Scheme" na

iv) Mpango wa kusimamia madeni ya nje (External Debt Management Strategy).

29. Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imekuwa ikitoa uzito sawa katika kushughulikia madeni ya ndani na nje na mara zote imekuwa ikijitahidi kulipa kulingana na uwezo wake. Hivyo, si kweli kwamba Serikali imekuwa ikiyapa kipaumbele madeni ya nje tu. Sera hii ya kulipa madeni kwa kulingana na uwezo wetu inaonyeshwa vizuri kwenye jedwali namba 7 la hotuba hii. Jedwali hilo linaonyesha jinsi tunavyolipa madeni yetu ya ndani na ya nje ukilinganisha uwezo wetu na kiasi tunachodaiwa kila mwezi tangu Julai 1997.

30. Aidha, katika hotuba yake kwa Taifa kuhusu madeni, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alielezea nia ya Serikali juu ya ulipaji madeni ya nje. Lengo lilikuwa kuonyesha kwa vitendo nia yetu ya kulipa madeni hayo ijapokuwa uwezo wetu ni mdogo.

Pia alielezea sababu za msingi ambazo ziliifanya Serikali kuonyesha nia hiyo. Baadhi ya sababu hizo ni pamoja na kujenga heshima na uaminifu wa Taifa letu, kujenga mahusiano na maelewano mazuri na wahisani na wakopeshaji ili watupunguzie mzigo wa madeni yetu ambayo tunawajibu wa kuyalipa, na kuweka mazingira bora kwa wawekezaji binafsi kutoka nchi za nje. Kutokana na juhudi hizo, nchi yetu imeendelea kupata misaada na mikopo kutoka nje ambayo imeelekezwa katika Sekta za huduma za jamii pamoja na zile za uzalishaji kama nilivyoeleza hapo awali wakati nikizungumzia misaada na mikopo kutoka nje.

**Maslahi ya Watumishi:**

31. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 1997/98, Serikali imefanya marekebisho ya mishahara ya watumishi wake katika ngazi mbali mbali ili angalau kupunguza makali yatokanayo na kupanda kwa gharama za maisha. Hata hivyo, Serikali inakiri kuwa marekebisho hayo hayalingani na hali halisi ya maisha kutokana na hali ya uchumi kuwa

duni, hivyo kusababisha Serikali kuwa na mapato madogo ambayo hayakidhi mahitaji ya Taifa. Serikali pia inaangalia namna ya kuboresha malipo ya pensheni kwa Viongozi wa Taifa, wanasiasa wengine na wafanyakazi wa umma kwa ujumla. Miswada ya kubadili sheria mbalimbali zinazohusika italetwa katika Bunge hili Tukufu kwa marekebisho yanayotakiwa.

**MISINGI NA SERA ZA BAJETI KWA MWAKA 1998/99:**

32. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo kuhusu tathmini ya bajeti ya mwaka 1997/98, napenda sasa nielezee misingi na sera za bajeti ya mwaka 1998/99. Misingi ya bajeti ya mwaka 1998/99 inalenga katika kufanikisha shabaha zifuatazo:

i) Kukuza pato la taifa kwa asilimia 3.5;

ii) Kuendelea kupunguza mfumuko wa bei hadi asilimia 7.5 ifikapo mwisho wa Juni, 1999;

iii) Kupunguza nakisi katika urari wa malipo na

nchi za nje kwa kukuza mauzo nje;

iv) Kuongeza ajira hasa katika sekta binafsi;

v) Kuimarisha utoaji huduma za Serikali kwa kuongeza ufanisi katika sekta mbalimbali;

vi) Kukuza sekta ya viwanda na kuvilinda kutokana na ushindani usiokuwa wa haki;

vii) Kuboresha usimamizi wa bajeti ya Serikali na kuongeza uwazi zaidi katika kukusanya mapato na kugawa fedha za matumizi;

viii) Kuweka utaratibu madhubuti utakaohakikisha kuwa deni la taifa haliongezeki zaidi ya uwezo wa kulipa;

ix) Kuongeza akiba ya ndani (domestic savings) ili kuweza kugharamia uwekezaji kutokana na raslimali ya ndani;

x) Kuweka mkakati wa kupunguza kiwango cha deni la taifa katika bajeti ya Serikali ili sehemu kubwa ya bajeti hiyo itumike kuboresha huduma za jamii na za kiuchumi; na

xi) Kukuza ushirikiano wa Afrika Mashariki, COMESA, SADC na uuzaji wa bidhaa zetu nje ya nchi yetu.

33. Kwa kuzingatia haya, Serikali katika mwaka wa fedha 1998/99 imeandaa sera za bajeti zinazolenga katika kufanikisha utekelezaji wa misingi hii katika muda wa kati (medium term). Nia ya Serikali ni kuona kuwa hatua muhimu za awali za utekelezaji zinachukuliwa katika mwaka huo wa fedha.

**Sera za Mapato:**

34. Mheshimiwa Spika, sera za mapato kwa mwaka 1998/99 zinalenga kuimarisha ukusanyaji mapato ya Serikali katika vianzio mbalimbali vya kodi. Lengo la

hatua hii ni kuhakikisha kuwa mapato ya Serikali kwa mwakani hayapungui Shs. 699,521 milioni sawa na asilimia 13 ya pato la taifa ikilinganishwa na matarajio ya Shs. 627,500 milioni sawa na asilimia 13 ya pato la Taifa kwa mwaka 1997/98. Ili kufikia kiwango hicho cha mapato na kwa kuzingatia madhara ya EL-NINO katika sekta za uzalishaji juhudi za ziada zinahitajika kwa TRA na Wizara mbalimbali ili kuhakikisha kuwa kiwango hicho cha mapato kinafikiwa. Juhudi hizi zinajumuisha kuanzishwa kwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), kuruhusu matumizi zaidi ya mabohari ya forodha, kuchunguza mfumo wa "tariff" kwa lengo la kupunguza wingi na viwango vyake. Hii pia inahusu utayarishaji wa misamaha ya kodi inayotambulika kisheria kuhamishiwa TRA.

35. Mheshimiwa Spika, Kodi ya Ongezeko la Thamani (Value Added Tax-VAT), itaanza rasmi Julai Mosi, 1998. Baadhi ya faida za kodi hiyo mpya nchini ni:

i) Kupanua wigo wa kodi ambao utaiwezesha

Serikali kuongeza mapato yatokanayo na kodi hivyo kuiwezesha kuboresha huduma kwa wananchi;

ii) Mfumo wa VAT utaboresha ufanisi na kurahisisha usimamizi wa kodi kutokana na matumizi ya kiwango kimoja (20%) na kuchukua nafasi ya kodi ya mauzo na kodi nyingine kadhaa (ushuru wa stamp na kodi ya starehe kwa wafanyabiashara watakaosajiliwa kulipa VAT;

iii) VAT itakuwa ni kichocheo cha uuzaji bidhaa nje ya nchi kutokana na kutoza kodi kwa kiwango cha asilimia sifuri (0%) kwenye bidhaa/huduma hizo na kuruhusu urejeshaji wa kodi iliyolipwa kwenye manunuzi ya bidhaa na huduma hizo;

iv) VAT itakuza uaminifu katika ulipaji wa kodi kwa kuwa wafanyabiashara watalazimika

kudai ankara za kodi (stakabadhi) sahihi kwenye manunuzi yao ili kujipatia marejesho makubwa ya kodi kwenye manunuzi na hivyo kupunguza kodi wanayostahili kulipa Serikalini.

Ili kufanikisha malengo yanayotarajiwa, Serikali inategemea ushirikiano thabiti kutoka kwa wafanyabiashara ikiwa ni pamoja na utunzaji wa kumbukumbu sahihi za biashara zao.

36. Mheshimiwa Spika, Serikali pia inakusudia kuruhusu uwekaji bidhaa zaidi kwenye mabohari ya Forodha (General Bonded Warehouses). Hivi sasa, baadhi ya bidhaa kama vyakula, nguo, n.k. haziruhusiwi kuhifadhiwa kwenye maghala ya aina hii. Utaratibu huu, umekuwa unaikosesha Tanzania soko muhimu katika nchi za jirani za Zambia, Malawi, Ruanda, Burundi, Uganda na Jamhuri ya Kongo. Marekebisho yanayopendekezwa katika eneo hili yatasaidia kukuza biashara kati ya Tanzania na nchi

jirani. Pamoja na hatua hiyo, Serikali itaimarisha udhibiti katika mabohari hayo ili hatua hii isiwe chanzo cha uvujaji wa kodi kama ilivyokuwa huko nyuma.

37. Mheshimiwa Spika, Serikali pia inakusudia kuchunguza mfumo wa "tariff" kwa lengo la kupunguza wingi wa viwango vilivyopo na hivyo kurahisisha usimamizi wake, ikiwa ni pamoja na kurejesha utaratibu wa viwango vya "tariff" kwa nchi za COMESA ili kuimarisha biashara katika nchi hizo.

38. Mheshimiwa Spika, ni nia ya Serikali pia kuhamishia TRA taratibu zote za utayarishaji wa misamaha ya kodi inayotambulika kisheria kama vile ya TIC, miradi ya Wahisani na Balozi mbalimbali pamoja na kuwataka wanaoomba misamaha ya kodi inayotolewa kwa ridhaa ya Waziri wa Fedha wawasilishe maombi yao kupitia Mamlaka ya Mapato. Aidha, utaratibu wa "Duty Draw Back" utafanyiwa marekebisho ili kodi inayokusanywa iwekwe kwenye Akaunti maalum badala ya kuingizwa kwenye Mfuko

Mkuu wa Serikali. Wauzaji nje warejeshewe kodi waliyolipa kutokana na akaunti hii baada ya kuthibitisha mauzo nje.

39. Mheshimiwa Spika, Serikali inakusudia kuchukua hatua zifuatazo, katika maeneo ya mapato yatokanayo na vianzio visivyo vya kodi:

i) Wizara zinazokusanya mapato mengi zitaruhusiwa kuendelea kubakiza sehemu ya mapato hayo (retention scheme) ili kuboresha shughuli za ukusanyaji mapato hayo. Hata hivyo, kuanzia mwaka wa fedha 1998/99, mapato yote yanayokusanywa na vyombo hivi yataingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwanza na kisha kupewa sehemu iliyokubalika kutokana na mapato hayo. Aidha, Hazina itaratibu kwa karibu zaidi matumizi ya fedha hizo za "retention" ili kuhakikisha kuwa zinatumika kulingana na makubaliano kati ya Hazina na Wizara inayohusika;

ii) Ada mbalimbali zitachunguzwa ili kuzihuisha. Aidha, uwezekano wa kupanua wigo wa utozaji ada katika maeneo ambayo hivi sasa hayatozwi ada utachunguzwa;

iii) Ada mbalimbali zinazototozwa na Serikali za Mitaa hasa kwenye bidhaa za viwandani na mazao ya kuuza nje zitachunguzwa kwa lengo la kuzioanisha (consolidate). Hatua hii itasaidia kupunguza bughudha kwa viwanda na makampuni yanayoshughulikia mazao ya biashara.

**Misaada na Mikopo ya Nje:**

40.Mheshimiwa Spika, katika eneo hili, Serikali inafahamu wazi kuwa jukumu la kujenga uchumi unaojitegemea ni la Watanzania wenyewe. Pamoja na ukweli huo, misaada ya nje inasaidia kutuongezea uwezo kwa muda wa kugharamia maendeleo yetu.

Hivyo, ni vyema misaada hiyo ikaelekezwa zaidi katika uwekezaji badala ya kutumika katika matumizi ya kawaida. Kwa kuzingatia shabaha hii, Serikali katika mwaka 1998/99 itachukua hatua zifuatazo:-

i) Kuendelea na mipango ya kurekebisha uchumi inayodhaminiwa na IMF na Benki ya Dunia;

ii) Kuendelea na majadiliano ya kila mwaka na Wahisani mbalimbali ili kutusaidia katika kuchangia gharama za miradi muhimu ya Serikali;

iii) Hazina kuchukua jukumu la kuratibu kwa karibu zaidi misaada inayopokelewa kati ya Wizara na Wahisani;

iv) Kuanzisha mfuko wa "Multilateral Debt Relief Fund" utakaochangiwa na Wahisani mbali mbali ili kusaidia kulipia madeni ya vyombo vya fedha vya kimataifa.

**Mikopo ya Ndani:**

41. Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa katika misingi ya bajeti ya mwaka 1998/99, Serikali inadhamiria kuendelea kupunguza mfumuko wa bei pamoja na kuongeza akiba ya ndani (domestic savings). Kwa maana hii, Serikali haitarajii kukopa, hasa kutoka kwenye mabenki kwa mwaka ujao bali itakuwa inapunguza deni lake. Aidha, Serikali itakopa kwa utaratibu wa dhamana za Hazina (Treasury Bills) ili kulipia dhamana zinazopevuka badala ya Serikali kutumia mapato yake. Kadhalika, mikopo yoyote mingine ya ndani isiyo ya mabenki ambayo Serikali italazimika kukopa itazingatia riba za dhamana za Hazina kama kigezo cha gharama halisi ya mikopo hiyo.

**Matumizi:**

42. Mheshimiwa Spika, hatua zinazotarajiwa kuchukuliwa katika eneo hili zina lengo la kuimarisha udhibiti na kuongeza uwazi katika matumizi ya Serikali. Kwa kuzingatia kuwa matumizi yaliyopangwa

hasa ya kawaida ni madogo kuliko mahitaji halisi, ni jambo la msingi sana kuimarisha udhibiti na kuongeza uwazi katika matumizi hayo. Hatua zinazotarajiwa kuchukuliwa ili kufanikisha azma hii ni pamoja na:-

i) Kuendelea kutumia utaratibu wa "Cash Budgeting". Ingawa fedha zitaendelea kutolewa kila mwezi, utaratibu huu utaboreshwa kwa kutoa matarajio ya mgao wa fedha kwa vipindi vya miezi mitatu mitatu. Utaratibu huu utasaidia vyombo hivyo kupanga vizuri matumizi yao. Ni muhimu ieleweke kuwa vyombo vya Serikali vitatakiwa kutumia tu kutokana na mgao wa kila mwezi. Viwango vya fedha vitakavyotolewa kwa miezi mitatu ni "indicative";

ii) Kuanzisha utaratibu wa kuingiza mihadi (commitments) kwenye matumizi ya baadhi ya Wizara. Utaratibu huu utasaidia sana

kupunguza kuwapo kwa malimbikizo ya madeni ya vifaa na huduma kwenye vyombo vya Serikali;

iii) Upangaji wa fedha za matumizi utazingatia utoaji fedha nyingi kwenye sekta za huduma za jamii na huduma za kiuchumi;

iv) Fedha zote za Mfuko wa barabara "Road Fund Tax" kuanzia mwaka 1998/99 zitatumika kwa ajili ya kugharamia matengenezo na ujenzi wa barabara tu;

v) Ugawaji wa fedha za matumizi kwa kila fungu utazingatia malengo ya kazi za utoaji huduma yanayotegemewa kufikiwa na Wizara inayohusika katika mwaka 1998/99;

vi) Malipo ya madeni ya nje na ndani yatazingatia uwezo wa kulipa. Kwa hiyo bado tutaendelea kulimbikiza malipo ya

madeni yaliyopevuka. Hata hivyo, madeni ya vyombo vya fedha vya kimataifa (Multilateral Institutions), madeni ya Paris Club na Wazabuni yatapewa kipaumbele katika malipo;

vii) Matumizi kwa ajili ya gharama za umeme kwa vyombo vya Serikali yametengwa Hazina. Chini ya utaratibu huu, Hazina italipa moja kwa moja kwenye Shirika la Umeme baada ya vyombo husika vya Serikali kuthibitisha matumizi yake;

viii) Kuzingatia mahitaji maalum ya kukabiliana na madhara yanayotokana na mvua za EL-NINO, jumla ya Sh.11,848.1 milioni zimetengwa kama ifuatavyo:-

- Barabara Sh.10,000.0 milioni

- Maji milioni Sh. 400.00

- Kilimo milioni Sh.1,448.1

Kwa kuzingatia Waraka wa Rais Na. 1 wa mwaka 1998 kuhusu kubana matumizi ya Serikali, kuanzia mwaka 1998/99 ununuzi wa magari yote ya Serikali utazingatia aina ya magari ya gharama nafuu yaliyosawazishwa. Aidha, utaratibu wa kununua samani kwa ajili ya ofisi na nyumba zote za Serikali unarekebishwa kwa lengo la kuweka viwango ambavyo vitatolewa na Wizara ya Ujenzi.

43. Mheshimiwa Spika, pamoja na ufinyu wa bajeti, sekta za jamii na uchumi zinaendelea kupewa umuhimu katika mwaka wa fedha wa 1998/99. Kwa mfano, uchambuzi wa mgao wa bajeti ya matumizi mengineyo (other charges - O.C.) unaonyesha uwiano ufuatao:-

- Huduma za jamii 24.0%
- Ulinzi na Usalama 22.6%
- Huduma za uchumi 20.1%
- Utawala 13.8%
- Uzalishaji 4.5%
- Matumizi maalum 15.0%

Wakati huo huo, kwa kuzingatia azma ya Serikali ya kuhamishia utekelezaji kwenye ngazi ya wilaya/halmashauri, bajeti ya mikoa imepungua sana. Katika mwaka 1998/99, Sekretariati za Mikoa zimetengewa Shs. 6,614.3 milioni kati ya Sh. 120,900 milioni au asilimia 5.5 tu ya bajeti za mikoa.

**Sekta ya Fedha:**

44. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 1998/99, Serikali imeazimia kuhakikisha kuwa mfumuko wa bei unashuka hadi chini ya asilimia kumi kwa kudhibiti ujazi wa fedha. Hii ni pamoja na Serikali kuendelea kupunguza deni lake kwa mabenki, kutumia kufuatana na mapato (cash budgeting) na kutokopa

kutoka mabenki. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kufanya marekebisho ya benki zetu kwa lengo la kuzifanya zitoe mchango katika kuinua uchumi wetu na kuzitayarisha kubinafsishwa.

45. Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali katika kurekebisha Sekta ya Fedha ikiwa ni pamoja na kukaribisha mabenki binafsi ya ndani na nje, ni kuleta ushindani katika ubora na unafuu wa bidhaa (products) zinazotolewa na mabenki hayo kwa wateja wake hasa mikopo yenye riba nafuu kwa ajili ya uwekezaji katika uchumi. Kwa misingi hiyo, bila ya kudhibiti mfumuko wa bei (to contain inflation), na kurekebisha mabenki ya umma ni vigumu kwa mabenki kuweza kupunguza viwango vya riba kwa mikopo inayotoa.

**Sekta ya Nje:**

46. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 1998/99, Serikali itaendelea na sera yake ya kukuza uchumi kwa kuitumia sekta ya nje kikamilifu. Serikali

itahamasisha uuzaji nje bidhaa na huduma mbalimbali pamoja na kuhakikisha ubora wa bidhaa hizo ili ziweze kuhimili ushindani uliopo katika soko la dunia ambako mataifa yenye viwango tofauti vya teknolojia hufanya biashara. Aidha, Serikali itaendelea na juhudi zake kwa kuzingatia maoni ya wauzaji na wanunuzi bidhaa nje ili kuzipunguza au kuondoa kabisa dosari mbali mbali ambazo zitaonekana kukwamisha biashara hizo. Vile vile, jitihada zitaendelea kuchukuliwa za kuweka mazingira mazuri ya kiuchumi, kukuza huduma mbalimbali muhimu, kuweka mifumo mizuri ya mawasiliano na kuhusisha sekta binafsi katika mtazamo mzima wa sekta hii muhimu.

**Sekta ya Mashirika:**

47. Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, ni nia ya Serikali kuendelea kupunguza utegemezi wa mashirika katika bajeti ya Serikali. Pamoja na kuendelea kuyaboresha mashirika hayo, hatua za makusudi ni lazima zichukuliwe ili kuongeza ufanisi. Hii ndiyo njia pekee ya kujitayarisha kuingia katika

ushindani na kupata bei nzuri pale yatakapobinafsishwa. Aidha, kwa yale mashirika yatakayoonekana kushindikana kurekebishwa au kuuzwa, Serikali itayafilisi ili fedha itakayopatikana iweze kulipa madeni yatakayokuwepo wakati huo kwa mujibu wa sheria ya ufilisi.

48. Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba Mfuko wa Ubinafsishaji (Privatisation Trust) uliundwa kwa sheria iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu mwezi Aprili, 1997. Ni vyema ikaeleweka wazi kuwa huu sio mfuko wa kutoa mikopo kwa ajili ya wananchi kununua hisa bali ni utaratibu ambapo hisa za Serikali zinazobakishwa wakati mashirika yanabinafsishwa zitashikiliwa mpaka hapo mashirika husika yatakapofuzu kuuza hisa zake kwenye Soko la Hisa (DSE). Waziri wa Fedha ameshatoa tamko rasmi katika Gazeti la Serikali kueleza tarehe na namna ya mfuko huo utakavyotumika. Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na PSRC inakamilisha uteuzi wa Bodi ya Udhamini (Board of Trustees) na Meneja wa Mfuko

ambaye kwa kawaida anatakiwa kuwa Taasisi ya Fedha ya hapa nchini.

**Sekta za Uzalishaji:**

49. Mheshimiwa Spika, uzalishaji katika kilimo, mifugo, viwanda, ufundi, madini, n.k. vinachangia kwa kiwango kikubwa pato la taifa hivyo kuleta hali nzuri ya maisha kwa wananchi. Kwa hiyo, Serikali itaendeleza sera zake za kuweka mazingira mazuri ambayo yatazidi kuimarisha sekta hii muhimu ya uzalishaji.

**Sekta Binafsi:**

50. Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kuimarisha sekta hii, Serikali itazidi kuweka sera na mazingira yanayovutia kwa sekta ya uzalishaji kwa lengo la kuongeza pato la taifa na hivyo kupunguza umaskini. Vile vile, Serikali itaendelea kutoa fedha kwenye mifuko ya Wanawake na Vijana na pia kwenye Shirika la National Income Generating Programme (NIGP) ili kuhamisisha miradi ya binafsi hapa nchini. Hivyo, kwa mwaka 1998/99,

Mfuko wa Wanawake na Vijana umetengewa Shs. 1.0 bilioni wakati Mfuko wa NIGP umetengewa Shs. 500 milioni.

**Sera za Madeni:**

51. Kuhusu Sera za Madeni, katika mwaka 1998/99, Serikali itaendelea na mikakati yake ya kupunguza mzigo wa madeni ya ndani na nje ya nchi. Kwa upande wa madeni ya nje, Serikali inategemea kuendelea na jitihada zake za kuzishawishi nchi mbalimbali wafadhili kuchangia mfuko wa kulipa madeni ya Taasisi za Fedha za kimataifa (Multilateral Debt Relief Fund) ili fedha za kutosha kulipia madeni hayo zipatikane, na kutoa nafuu zaidi katika bajeti ya Serikali na pia kuboresha huduma katika sekta za jamii.

52. Aidha, kufuatia kusainiwa kwa mkataba wa Paris Club hapo Januari 21, 1997 Serikali itaendelea kutekeleza maazimio yaliyokubaliwa katika mkataba huo ikiwa ni pamoja na kukamilisha mikataba na nchi

za wanachama wa Paris Club. Vile vile Serikali itaendelea na jitihada za kuanzisha mazungumzo na nchi ambazo si wanachama wa Paris Club ili kupata muafaka wa jinsi ya kupunguza deni.

53. Pamoja na juhudi hizo, Serikali itaendelea kutekeleza mpango wa kununua malimbikizo ya madeni ya kibiashara (Debt Buyback) yanayokadiriwa kufikia Dola za kimarekani 350 milioni. Chini ya utaratibu huu, Serikali inategemea kutumia fedha za msaada kutoka Shirika la Maendeleo la Benki ya Dunia (IDA) pamoja na nchi wahisani kulipia madeni haya.

54. Kwa upande wa madeni ya ndani, Serikali katika mwaka 1998/99 itaendelea na utaratibu wa kubadilisha madeni yaliyo na viwango vikubwa vya riba, kuwa madeni mapya yenye viwango vidogo (debt securitization) ili kupunguza gharama za malipo. Ili kupata ufumbuzi wa kudumu wa madeni yetu, Serikali iliunda Tume iliyoshughulikia kuandaa mkakati wa

kitaifa wa kupunguza madeni (National Debt Strategy). Tume hii imeshakamilisha kazi yake na kuwasilisha taarifa yake Serikalini. Serikali itaipitia taarifa hii kwa lengo la kutekeleza mapendekezo yake.

**Ushirikiano katika EAC, COMESA, na SADC:**

55. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 1998/99, Serikali imedhamiria kuendeleza juhudi zilizopo za kuleta mabadiliko ya maendeleo ya uchumi katika nchi za Afrika ya Mashariki na pia katika shirikisho la SADC na COMESA. Tathmini ya ushiriki wetu kwa wakati mmoja katika vyombo vyote viwili vya SADC na COMESA itafanywa ili tulinganishe faida za kushiriki kwenye mashirika yote mawili na zile za kuwa kwenye shirika moja tu.

**MFUMO WA BAJETI YA MWAKA 1998/99:**

56. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya Sera za bajeti, napenda sasa nielezee mfumo wa bajeti kwa mwaka 1998/99. Kwa kuzingatia sera hizo, na bila kufanya marekebisho ya mfumo wa kodi

uliopo, Serikali inatarajia kukusanya jumla ya Shs. 695,165.9 milioni za mapato ya ndani ili kugharamia bajeti yake.

57. Kwa upande wa matumizi, jumla ya Shs. 1,007,786 milioni zimekisiwa kutumika mwaka wa fedha 1998/99. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 74.0 ya mahitaji halisi ya Shs. 1,359,785.2 milioni kama yalivyowasilishwa na vyombo vya Serikali. Kwa maana hii, bado makisio ya matumizi hayatoshelezi mahitaji halisi ya muundo wa Serikali. Hivyo, Serikali inalazimika kuendelea kuchukua hatua za kupunguza majukumu yake iii yawiane na uwezo wa kuyagharamia. Aidha, juhudi zilizoelezwa hapo awali za kupunguza mzigo wa deni la taifa zitasaidia kupata fedha za kuongeza katika kugharamia muundo wa Serikali.

58. Kwa kuzingatia mapato yaliyoelezwa na kiwango cha matumizi kinachopendekezwa, pengo la shs. 312,620.1 milioni linajitokeza. Kutokana na kuendelea

kuwa na uhusiano mzuri na Wahisani wa nje, inakisiwa kuwa katika mwaka 1998/99 watasaidia Tanzania kwa kiasi cha shs. 309,265 milioni katika bajeti yake. Kati ya fedha hizo, Shs. 80,265 milioni ni za msaada wa "Import Support" na "Balance of Payment Support" na shs. 229,000 milioni ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kiwango hiki cha msaada kinapunguza pengo hadi kufikia shs. 3,355.1 milioni.

59. Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa hapo mwanzo kuhusu mikopo ya ndani, Serikali katika mwaka 1998/99 inategemea kupunguza limbilikizo la madeni ya vyombo vya fedha na visivyo vya fedha kwa kiasi cha Shs. 10,000 milioni. Azma hii inaongeza pengo na kufikia Shs. 13,355.1 milioni. Kutokana na jitihada za kubinafsisha Mashirika ya Umma, Serikali katika mwaka 1998/99 inatarajia kupata Shs. 9,000 milioni ili kusaidia bajeti yake. Kiasi hiki cha mapato kitapunguza pengo hadi kufikia Shs. 4,355.1 milioni ambazo itabidi zitafutiwe njia mpya za mapato.

**Hatua za Mapato Mapya**

60. Mheshimiwa Spika, marekebisho ya mfumo wa kodi pamoja na hatua mpya za mapato zinazopendekezwa zinalenga katika kuipatia Serikali jumla ya Sh.4,355.1 milioni ili kujaza pengo lililojitokeza. Hii ni pamoja na kutafuta mapato ya ziada na kufanya marekebisho ya mfumo wa kodi utakaosaidia kukuza na kuimarisha uchumi na mapato ya Serikali. Naomba hapa nichukue fursa hii kuipongeza Task Force ya Mapato ambayo kwa mara nyingine tena imesaidia sana Serikali katika kuchunguza mfumo wa kodi na kutoa mapendekezo mazuri kwa Serikali. Sera za kodi na hatua za mapato mapya zinazingatia marekebisho katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kuanzishwa kwa Kodi Mpya ya Kodi ya ongezeko la thamani yaani Value Added Tax (VAT);

(ii) Marekebisho ya mfumo wa Ushuru wa Forodha (Customs Tariff Act No.12 of 1976);

(iii) Marekebisho kwenye kodi ya mauzo nje (Export Tax);

(iv) Uuzaji nje wa Chuma chakavu;

(v) Marekebisho ya kodi kwenye Bia, Sigara, Pombe kali, Mvinyo, Chibuku na Vinywaji Baridi;

(vi) Marekebisho ya kodi za mafuta ya petroli;

(vii) Marekebisho ya kodi za magari;

(viii) Marekebisho katika sheria ya kodi ya mapato;

(ix) Kuhamasisha soko la mitaji;

(x) Marekebisho ya ada na "charges" mbali mbali zinazokusanywa na Wizara na Mikoa;

(xi) Kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji kodi (Improving Tax Administration);

(xii) Kurekebisha Sheria mbali mbali za kodi ili kuzihuisha na kuziwianisha;

(xiii) Marekebisho ya misamaha ya kodi isiyo ya lazima.

**Uanzishaji wa Kodi ya VAT**

61. Mheshimiwa Spika, kutokana na kupitishwa kwa Sheria ya VAT mwaka jana, kodi hii itaanza kutozwa rasmi Julai 1, 1998. Kutokana na kuanzisha kodi hiyo, kodi zifuatazo zinarekebishwa:-

(a) Kodi ya mauzo kwa bidhaa na huduma inafutwa kuanzia Julai 1, 1998.

(b) Ushuru wa stempu kwenye stakabadhi

(receipts based) kwa wafanyabiashara waliosajiliwa kwenye kodi ya VAT haitatozwa.

(c) Kodi ya starehe (Entertainment tax) kwa wafanyabiashara waliosajiliwa kwenye kodi ya VAT haitatozwa.

62. Pamoja na hatua hiyo, inapendekezwa kufanya marekebisho yafuatayo kwenye Sheria ya VAT ya mwaka 1997:-

(a) Baadhi ya huduma za Utalii kama vile kuangalia wanyama (Game viewing) n.k zisamehewe kodi ya VAT.

(b) Bidhaa za uwekezaji zinazohitaji muda mrefu kuwekezwa kabla uzalishaji kuanza, ziwe na taratibu tofauti za kulipa VAT. Utaratibu huo uwe wa aina ya kutoa mkopo (credit) kwa wahusika mpaka hapo uzalishaji utakapoanza.

(c) Wazalishaji na wafanyabiashara wenye bidhaa (stocks) ikiwa ni malighafi na bidhaa zote zilizonunuliwa kuanzia Januari 1998 au baada ya hapo ambazo zimelipiwa kodi ya mauzo watarejeshewa kodi hiyo iliyolipwa wakati watakapotozwa VAT.

(d) Nafaka zote na unga vitasamehewa kodi ya VAT kama ilivyoelezwa kwenye nyongeza ya pili (second schedule) ya Sheria ya VAT.

(e) Malighafi na vifungashio (Packaging materials) kwa ajili ya kutengeneza madawa zitasamehewa kodi ya VAT.

(f) Ili kusaidia wauzaji nje na walipa kodi wengine wa *VAT* waweze kufanya shughuli zao kwa ufanisi zaidi, marejesho *(refunds)* ya kodi walizolipa yafanyike katika muda wa mwezi mmoja baada ya kuwasilisha maombi ya marejesho ya kodi yao.

(g) Marejesho ya kodi ya *VAT* kwa wanaohusika yahusishe kodi hiyo na deni la kodi lililokubalika kwa pande zote mbili.

Hatua ya kuanzisha kodi ya *VAT*, kufuta baadhi ya kodi na kufanya marekebisho ya Sheria ya *VAT*, zinategemewa kuipatia Serikali mapato ya ziada ya Sh.6,635.1 milioni.

**Mfumo wa Ushuru wa Forodha**

63. Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kuwa mfumo wa viwango vya Ushuru wa Forodha urekebishwe ili uzingatie hatua ya usindikaji (Processing) iliyofikiwa yaani viwango vya chini kwa bidhaa za uwekezaji na malighafi, viwango vya kati kwa bidhaa zilizosindikwa kwa kiasi (semi-finished goods) na viwango vya juu kwa bidhaa zilizokamilika (finished goods). Hata hivyo, kutokana na kazi kubwa inayotakiwa kufanyika katika zoezi hili, marekebisho haya yanategemewa kukamilika Desemba 1998 na mfumo mpya kuanza kutumika mapema iwezekanavyo. Mapendekezo haya

hayategemiwi kupunguza mapato ya Serikali kwa mwaka 1998/99.

### Viwango vya Ushuru wa Nchi za COMESA

64. Mheshimiwa Spika, kimsingi inapendekezwa kuwa, Tanzania ikubaliane tena na utaratibu wa *COMESA* na katika mwaka 1998/99 ipunguze viwango vya ushuru wa forodha kwa asilimia 80 kwa ajili ya bidhaa kutoka nchi za *COMESA*. Hata hivyo, kiwango hiki kisiongezwe hadi kufikia asilimia 90 ifikapo mwezi Oktoba 1998 kama masharti ya COMESA yanavyotaka. Hii ni kutokana na sababu kuwa itakuwa vigumu kubadilisha viwango vya kodi katikati ya mwaka wa fedha.

65. Ili kuendelea kulinda viwanda ambavyo bado ni vichanga sana, inapendekezwa kuweka ushuru wa ziada *(suspended duty)* wa asilimia **20** kwa bidhaa kutoka nchi za *COMESA* ambazo ni tishio kwa viwanda hivyo. Sambamba na hatua hii, Serikali itatilia mkazo suala la *'Rules of origin'* kama inavyotakiwa katika utaratibu wa *COMESA*.

66. Mheshimiwa Spika, kwa bidhaa za bia, vinywaji vikali, sigara na saruji, viwango vya sasa vya ushuru wa forodha na kodi nyingine vitaendelea kutozwa kwa nchi za *COMESA* na zisizo za *COMESA*. Aidha, inapendekezwa kuwa viwanda mbali mbali katika nchi za *COMESA* vinavyotaka kuuza bidhaa zao katika soko la Tanzania kwa utaratibu wa viwango vya *COMESA*, watatakiwa wateue wakala *(Agents)* hapa nchini kwa bidhaa hizo ambao watasajiliwa na *TRA* kwa ajili ya ulipaji kodi. Bidhaa zitakazoingizwa nchini nje ya mkondo huu zitakamatwa na kufungiwa. Hatua hizi zinategemewa kulinda mapato ya Serikali.

**Kodi ya Mauzo Nje (Export Tax)**

67. Mheshimiwa Spika, kutokana na sababu za msingi za kukuza mauzo nje, inapendekezwa kuwa kodi ya mauzo nje kwa mazao ya Pamba, Katani, Pareto, Korosho, Kahawa, Chai na Tumbaku ifutwe. Hatua hii itapunguza mapato ya Serikali kwa Sh.5,780.0 milioni.

**Uuzaji Nje wa Chuma Chakavu**

68. Mheshimiwa Spika, kufuatia malalamiko mengi kutoka kwa wafanyabiashara wa Chuma Chakavu, inapendekezwa kuruhusu tena uuzaji nje wa chuma chakavu. Hata hivyo, wauzaji hao watatakiwa kulipa kodi ya mauzo nje (export tax) ili kudhibiti uuzaji nje wa chuma chakavu ambacho ni malighafi muhimu kwa viwanda vya chuma hapa nchini. Wizara ya Viwanda na Biashara itasimamia biashara hii.

**Marekebisho ya Kodi kwenye Bia, Chibuku, Sigara, Pombe Kali/Mvinyo na Vinywaji Baridi**

69. Mheshimiwa Spika, kuhusu kinywaji cha bia, inapendekezwa kuwa ushuru wa bidhaa kwa bia zinazotengenezwa hapa nchini uwe Sh.**174.00** kwa lita na kodi ya *VAT* iwe asilimia **20**. Bia zinazotoka nchi za *COMESA* zitatozwa ushuru wa forodha wa asilimia **10**, ushuru wa bidhaa **Sh.195.00** kwa lita na kodi ya VAT asilimia **20**. Kwa upande wa bia za nje kutoka nchi zisizo za *COMESA* inapendekezwa kutoza ushuru wa forodha wa asilimia **30**, ushuru wa bidhaa wa

Sh.**153.00** kwa lita na kodi ya *VAT* asilimia **20**. Kuhusu pombe ya chibuku, inapendekezwa kuwa ushuru wa bidhaa wa Sh.**2.20** kwa lita unaotozwa hivi sasa ufutwe na badala yake kodi ya ongezeko la thamani *(VAT)* asilimia **20** itozwe. Lengo la hatua hii ni kuongeza ushuru wa bidhaa kwa bia kwa kiasi cha asilimia **5**.

**Sigara**

70. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sigara, inapendekezwa kufanya marekebisho ya viwango vya kodi mbali mbali kwa kila sigara 1,000 kama ifuatavyo:-

(a) Sigara zenye urefu wa *mm* **70** zinazozalishwa nchini zitozwe ushuru wa bidhaa Sh.**7,568.00** na kodi ya *VAT* asilimia **20**. Kwa sigara zenye urefu chini ya *mm* **70** zitozwe ushuru wa forodha wa Sh.**3,229.00** na kodi ya *VAT* asilimia **20**.

(b) Sigara zinazoagizwa kutoka nje ya nchi zitatozwa ushuru wa bidhaa wa Sh.**17,020.00**, ushuru wa forodha asilimia **30**, na kodi ya *VAT* asilimia **20**.

Hatua hizo zitaongeza ushuru wa bidhaa kwenye sigara kwa asilimia **5**.

**Pombe Kali na Mvinyo**

71. Mheshimiwa Spika, kuhusu pombe kali pamoja na mvinyo vinavyotengenezwa hapa nchini, inapendekezwa kuwa pombe kali zitozwe ushuru wa bidhaa Sh.**864.00** kwa lita pamoja na kodi ya *VAT* asilimia **20**. Mvinyo utatozwa ushuru wa bidhaa wa Sh.**508.30** kwa lita na kodi ya *VAT* asilimia **20**. Aidha, kwa bidhaa kama hizo zinazoagizwa kutoka nje, pombe kali itozwe ushuru wa forodha asilimia **30**, ushuru wa bidhaa wa Sh.**1,040.00** kwa lita na kodi ya *VAT* asilimia **20**. Kuhusu mvinyo unaoagizwa nje, ushuru wa forodha utakuwa asilimia **30**, ushuru wa bidhaa wa Sh.**776.00** kwa lita na kodi ya *VAT* asilimia **20**.

**Vinywaji Baridi**

72. Mheshimiwa Spika, Serikali inapendekeza kuwa vinywaji baridi vinavyozalishwa hapa nchini vitozwe kodi ya *VAT* asilimia **20** na ushuru wa bidhaa wa Sh.**43.00** kwa lita. Aidha, vinywaji baridi vinavyotoka nje vitozwe ushuru wa forodha asilimia 30, kodi ya *VAT* asilimia **20** na ushuru wa bidhaa wa Sh.**140.00** kwa lita. Hatua hizi zinalenga katika kulinda mapato ya Serikali yasipungue.

**Bidhaa za Karatasi**

73. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa bidhaa za karatasi, inapendekezwa kufutwa kwa misamaha ya kodi iliyokuwa ikitolewa kwa mujibu wa GN 122 na 142. Hatua hii inachukuliwa baada ya kuwa na uhakika kwamba wenye viwanda vya mag' eti wamekwishapata uwezo wa kujiimarisha.

**Marekebisho ya Kodi za Mafuta ya Petroli**

74. Mheshimiwa Spika, ili kuepuka matatizo kwenye

uchumi, inapendekezwa kuwa:-

(i) Aina zote za mafuta ya petroli zisamehewe kodi ya *VAT* lakini ziendelee kutozwa kodi nyingine.

(ii) Kwa kuwa kodi ya mauzo imefutwa, kodi ya aina hii iliyokuwa ikitozwa kwa bidhaa za mafuta ya petroli iunganishwe kwenye ushuru wa bidhaa ili kulinda mapato ya Serikali. Kutokana na pendekezo hili, kodi kwa aina mbali mbali za mafuta ya petroli zitakuwa kama ifuatavyo:-

**Ushuru wa Bidhaa *(Excise Tax)***

| | | | |
|---|---|---|---|
| (a) | LPG | - | Sh.**44.1372** kwa kilo |
| (b) | MSP | - | Sh.**64.2978** kwa lita |
| (c) | MSR | - | Sh.**58.4214** kwa lita |
| (d) | JET - AI | - | Sh.**24.0848** kwa lita |
| (e) | IK | - | Sh.**19.9451** kwa lita |
| (f) | GO | - | Sh.**16.8786** kwa lita |
| (g) | IDO | - | Sh.**14.0680** kwa lita |
| (h) | FO | - | Haina kodi. |

**Ushuru wa Barabara (Road Fund Tax)**

75. Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kubadilisha jina la *'Road Toll'* kuwa *'Road Fund Tax'* ili kuoanisha na matumizi yake. Aidha, kiwango cha sasa cha Ushuru wa Barabara *(Road Toll)* cha Sh.**70.00** kwa lita kwa mafuta ya MSP, MSR na GO kitaendelea kutumika kwa mwaka 1998/99. Hatua hizi hazitegemewi kuongeza mapato ya Serikali.

**Marekebisho ya Kodi za Magari**

76. Mheshimiwa Spika, kutokana na kodi ya magari madogo ya abiria *(Passenger Cars)* kuwa kubwa sana, inapendekezwa kuwa ushuru wa bidhaa kwa magari madogo yenye ukubwa wa *'engine'* isiyozidi **CC 2000** ufutwe. Ushuru wa forodha uwe asilimia **30** na kodi ya ongezeko la thamani *VAT* iwe asilimia **20**. Aidha, kwa magari madogo ya abiria yenye ukubwa wa *'engine'* zaidi ya *CC* **2000**, ushuru wa forodha uwe asilimia **30**, ushuru wa bidhaa asilimia **10** na kodi ya ongezeko la thamani *(VAT)* asilimia **20**.

77. Kuhusu magari ya aina ya *Pick-up*, malori na mabasi, inapendekezwa kuwa ushuru wa forodha uwe asilimia **20** na kodi ya ongezeko la thamani asilimia **20**. Magari makubwa yasiyounganishwa *(Completely Knocked Down - CKD)* yatatozwa ushuru wa forodha wa asilimia **5**, na kodi ya ongezeko la thamani asilimia **20**. Aidha, kwa magari yaliyotumika *(used passenger cars)*, inapendekezwa kuwa kiwango cha ushuru wa forodha kiwe asilimia **30** au Sh.**1.0** milioni kwa gari kutegemea na ipi ni kubwa, pamoja na kodi ya VAT asilimia **20**.

**Ushuru wa Magari kutoka nchi za Kigeni**

78. Inapendekezwa kupunguza ushuru wa kodi kwa magari kutoka nje ya Tanzania uwe Dola za Kimarekani 20 kwa kipindi kisichozidi mwezi mmoja badala ya Dola za Kimarekani 60 kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu ya sasa.

**Marekebisho ya Misamaha ya Kodi katika magari**

79. Mheshimiwa Spika, kutokana na kupunguza kodi za magari, inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye misamaha ya kodi katika magari yanayonunuliwa na Watumishi wa Serikali na wafanyakazi wengine pamoja na wananchi wanaorejea nchini *(Returning Residents)* ambao walikuwa wakilipa kodi ya asilimia **5**. Kuanzia Julai Mosi 1998 watatakiwa kulipa kodi za ongezeko la thamani *(VAT)* asilimia **20** na kwamba ushuru wa forodha pamoja na ushuru wa bidhaa unafutwa. Aidha, magari yatakayohusika na nafuu hii ya kodi ni magari madogo ya abiria *(passenger cars)* yenye ukubwa wa 'engine' usiozidi **CC 3000**. Magari madogo ya abiria *(passenger cars)* yenye ukubwa wa 'engine' zaidi ya **CC 3000** yatalipiwa kodi zote.

80. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa magari madogo *(Passenger Cars)* kwa wawekezaji hapa nchini ambayo yalikuwa hayalipiwi kodi chini ya utaratibu wa uwekezaji *(TIC)* hayahusiki na uzalishaji,

inapendekezwa kuwa yaondolewe katika orodha ya vivutio vya kuhamasisha uwekezaji na yalipiwe kodi zote.

81. Mheshimiwa Spika, hatua za kurekebisha kodi mbali mbali za magari hazitegemei kupunguza mapato kwa sababu magari mengi yamekuwa hayalipiwi kodi kutokana na misamaha mbalimbali. Aidha, marekebisho haya yatasaidia sana wananchi kununua magari mapya na hivyo kupunguza gharama za matengenezo na vipuri ambazo ni mzigo kwa taifa kutokana na mahitaji ya fedha za kigeni kuagizia vipuri.

**Marekebisho ya Kodi ya Matairi ya Magari**

82. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matairi ya magari, matairi ya aina ya radial, inapendekezwa yatozwe ushuru wa forodha wa asilimia 20 badala ya asilimia 30 ya sasa na kodi ya ongezekoa la thamani ya asilimia 20. Kwa matairi ya aina nyingine, ushuru wa forodha utabaki kuwa asilimia 30 kama ilivyo sasa na kodi ya ongezeko la thamani ya asilimia 20.

**Hatua za Kodi zenye lengo la kulinda Viwanda**

83. Mheshimiwa Spika, ili kulinda viwanda vyetu vya hapa nchini kutokana na ushindani usiohaki *(unfair competition)* yafuatayo yanapendekezwa:-

(a) Madawa ya kutengeneza nguo ya *dyes, acids* na mengineo yatatozwa ushuru wa forodha wa asilimia **5** badala ya kiwango cha asilimia **10** cha sasa.

(b) Malighafi za kutengenezea betri za magari zenye *"tariff No"*. zifuatazo ziwe na ushuru wa forodha wa asilimia **5**:-

| | Item | Tariff No. |
|---|---|---|
| (i) | Battery cases (plasticised or rubberised) | 3923.10.00, 4016.99.90 |

| | | |
|---|---|---|
| (ii) | Stoppers, Lids, Caps etc. | 3923.50.00, |
| | | 4016.99.90 |
| (iii) | Sulphuric Acid | 2851.00.00 |
| (iv) | Lead | 7806.00.90 |
| (v) | Cadmium | 8107.90.00 |

(c) Malighafi ya kutengeneza mafuta laini (lubricants) yenye tariff No. 2710.00.90 na 3811.21.90 zitozwe ushuru wa forodha wa asilimia 5 badala ya asilimia 10 ya sasa.

84. Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kuwa, ushuru wa forodha unaotozwa kwa mali ghafi kwa ajili ya uzalishaji bidhaa za kuuza nje *(exports)* sasa utalipwa kwenye Akaunti maalum ya *TRA* badala ya kuingizwa kwenye Akaunti ya Mlipaji Mkuu wa Serikali *(Pay Master General - PMG).* Hatua hii inalenga

kuondokana na matatizo yaliyojitokeza kwenye utaratibu wa *"Duty Drawback Scheme"*. Halmashauri ya Biashara Nje ambayo kwa sasa husimamia na kuratibu marejesho haya haitahusishwa tena katika utaratibu huu mpya. Hatua hizi hazitegemewi kupunguza mapato ya Serikali.

**Bidhaa zilizokamilika (Finished Products)**

85. Mheshimiwa Spika, ili kuweka mazingira sawa ya ushindani kati ya bidhaa zinazoagizwa na zinazotengenezwa hapa nchini inapendekewa kuwa vifungashio ambavyo matumizi yake ni ya kurudiwa *(Repetitive)* vitozwe ushuru wa forodha asilimia **30** na vifungashio ambavyo matumizi yake si ya kurudia *(Non- Repettitive)* vitozwe ushuru wa forodha wa asilimia **20**. Bidhaa za viatu, magunia *(P.P. Bags)*, nguo na vitambaa (mpya na mitumba), mchele, mafuta ghafi na yaliyosafishwa ya kula, sukari na unga wa ngano zifanyiwe ukaguzi kabla hazijaingizwa nchini *(Pre-Shipment Inspection)* bila kujali thamani ya bidhaa hizo isipokuwa mitumba. Aidha, sukari

inayotumika kama malighafi kwa viwanda vya Soda na Bia itatozwa ushuru wa forodha wa asilimia 10 bila kuwataka watumaiaji kuweka asilimia 20 zaidi ambayo baadaye kurejeshwa kama utaratibu wa sasa unavyotaka. Hatua hizi hazitegemewi kupunguza mapato.

**Kutoza Ushuru wa Stampu kwa Mifuko ya NPF na PPF**

86. Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kutoza ushuru wa stampu mifuko ya National Social Security *Fund (NPF)* na *PPF* kwa mapato yatokanayo na biashara zinazofanywa na mifuko hiyo isipokuwa kwa michango ya wanachama. Hii ni kutokana na sababu kuwa shughuli za mifuko hii kwa sasa zimepanuka na kujihusisha na biashara kama vyombo vingine vya kibiashara.

**Marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Mapato (Income Tax Act 1973)**

87. Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kufanya

marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Mapato *(Income Tax Act Of 1973)* kwa lengo la kuleta nafuu kwa walipaji, kuongeza mapato ya Serikali, pamoja na kurahisisha ukusanyaji kama ifuatavyo:-

(a) **Kutozwa Kodi ya Mapato Mifuko ya NPF na PPF**

Inapendekezwa kutoza kodi ya mapato *(Corporation Tax)* mifuko hii kwa mapato ya ziada yatokanayo na biashara bila kuhusisha na michango ya wanachama wa mifuko hiyo. Hii ni kutokana na sababu kuwa shughuli za mifuko hii kwa sasa zimepanuka na kujihusisha na biashara kama vyombo vingine vya kibiashara.

(b) **Kodi ya Mafao ya Nyumba *(Housing Benefits Tax)***

Inapendekezwa kuwa kodi hii irekebishwe na kuwa asilimia **15** ya mshahara pamoja na marupurupu ili kuondoa usumbufu na kurahisisha ukusanyaji.

(c) **Nafuu ya Kodi kwa Watu Binafsi *(Personal Relief Allowances)***

Kutokana na matatizo kuhusu upatikanaji wa nafuu hii ya kodi pamoja na thamani ndogo ya nafuu yenyewe, inapendekezwa kuwa nafuu ya kodi kwa watu binafsi ifutwe. Hatua hii haitaongeza mapato kwa sababu walipa kodi wengi wamekuwa hawadai nafuu hii.

(d) **Kodi ya Zuio kwa Bidhaa na Huduma *(Withholding Tax on Goods and Services)***

Inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye kodi hii ili kuondoa usumbufu kwa wanaotakiwa kuikusanya:-

(i) Kiwango cha chini kwa ajili ya kodi hiyo kiwe Sh.**100,000** kwa *'transaction'*.

(ii) Serikali itaangalia uwezekano wa kufuta kodi ya zuio kwa bidhaa na huduma katika mwaka 1999/2000 baada ya kuanzisha *'Tax Payers Identification Number' (TIN)*.

(iii) Kodi ya Zuio iwe kwa manunuzi ya bidhaa na huduma bila kujumuisha kodi ya *VAT* iliyolipwa.

(e) **Kodi Nyingine za Zuio *(Other Withholding Taxes)***

Inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye baadhi ya kodi nyingine za Zuio ili kutoa nafuu kwa walipaji wake. Mapendekezo hayo ni:-

(i) Kodi ya zuio kwa mrahaba *(royalties)*ipunguzwe kutoka asilimia **30** za sasa hadi asilimia **20**. Hatua hii inalengo la kuoanisha viwango vya kodi hii na nchi nyingine za Afrika Mashariki.

(ii) Kodi ya Zuio kwa ndege za kukodi *(Leased Aircraft)* ipunguzwe kutoka asilimia **40** hadi asilimia **10**. Hatua hii inalengo la kupunguza mzigo wa gharama za kukodi ndege kwa ajili ya kuimarisha usafiri wa anga kwa makampuni ya ndege ya hapa nchini.

(iii) Kodi ya zuio kwa mali isiyohamishika inayomilikiwa na wasio wakazi *(non-resident)* ishushwe kutoka asilimia **40** na kuwa asilimia **20**.

(iv) Kodi ya Zuio kwa wataalam ambao sio wakazi *(non resident withholding tax on management and professional fees)* ipunguzwe kutoka asilimia **30** hadi asilimia **20**. Hatua hii inalengo la kupunguza mzigo wa kodi kwa wahusika.

Hatua za marekebisho katika kodi ya zuio haitegemewi kuathiri mapato ya Serikali lakini zitaongeza *'compliance'*.

(f) **Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato kwa wenye shahada ya TIC**

Inapendekezwa kubadilisha kifungu kinachoruhusu asilimia 100 ya gharama za uwekezaji kupunguzwa kwenye kukadiria kodi ya mapato na badala yake kutumia viwango vinavyotumika kwa sasa kwenye Jedwali Na. 2 la Sheria ya Kodi ya Mapato. Lengo la hatua hii ni kuwianisha na viwango vya kodi vinavyotozwa na nchi jirani.

**Soko la Mitaji (Capital Markets and Securities)**

88. Mheshimiwa Spika, ili kuhamasisha Soko la Mitaji, inapendekezwa kufanya marekebisho ya kodi ya mapato katika eneo hili ili kuhamasisha na kuendeleza

soko hili. Hivyo inapendekezwa kuwa, mapato yatokanayo na gawio kutoka kwenye kampuni zilizosajiliwa kwenye soko la mitaji yatozwe asilimia **5** kama kodi ya zuio *(Withholding tax)*. Hatua hii inalenga katika kuhamasisha watu binafsi kununua hisa kwenye soko la mitaji.

**Kuimarisha Usimamizi wa Ukusanyaji Kodi (Improving Tax Administration)**

89. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji kodi *(improving tax administration)*, yafuatayo yanapendekezwa:-

(a) Ili kuimarisha ukaguzi wa Bidhaa zinazoingizwa nchini, inapendekezwa kufanya marekebisho katika mkataba wa Kampuni ya *SGS* ili kuruhusu ukaguzi *(Pre-shipment Inspection)* wa bidhaa zote zinazoingizwa Tanzania Bara kupitia Tanzania Visiwani.

(b) Vile vile inapendekezwa kuangalia upya sheria mbali mbali za kodi kwa lengo la kuwianisha viwango vya faini na adhabu za makosa ya kutolipa kodi *(tax penalties and fines)*.

(c) Pia, ili kukuza biashara kati ya Tanzania na nchi jirani, inapendekezwa kuwa mabohari ya forodha *(General Bonded Warehouses)* yaruhusiwe kwa bidhaa zote. *TRA* inaendelea kuimarisha usimamizi wa mabohari hayo.

(d) Aidha, misamaha ya kodi kwa bidhaa za uwekezaji na nyinginezo itatazamwa upya kwa lengo la kuipunguza baada ya kufanya uchambuzi wa mfumo wa ushuru wa forodha katika mwaka ujao wa fedha kama ilivyoelezwa hapo awali.

(e) Kwa upande wa Rufaa ya Kodi, inapendekezwa kuwa Sheria ya *TRA* na Sheria za Kodi mbali mbali zirekebishwe ili kuruhusu kuundwa kwa chombo kimoja cha Rufaa ya Kodi. Hatua hii itasaidia kuondoa usumbufu kwa walipa kodi.

**Marekebisho ya Ada na 'Charges' Mbali mbali zinazokusanywa na Wizara na Mikoa**

90. Mheshimiwa Spika, inapendekezwa pia kufanya marekebisho ya ada na *'charges'* mbali mbali zinazokusanywa na Wizara na Mikoa ili kuzihuisha pamoja na kuziwianisha. Pendekezo hili litaipatia Serikali mapato ya ziada ya kiasi cha Sh.**3,500.0** milioni.

91. Mheshimiwa Spika, kutokana na kuanzisha kodi ya VAT na kuhusika kwa kodi hiyo na marekebisho ya kodi nyingi zinazopendekezwa, hatua zote za mapato zilizopendekezwa zitaanza kutekelezwa rasmi kuanzia Julai 1, 1998.

**Muhtasari wa Mapato Kutokana na Hatua Mbalimbali za Kodi kwa Mwaka 1998/99:**

92. Mheshimiwa Spika, kutokana na hatua mbali mbali za kurekebisha mfumo wa kodi na kuimarisha ukusanyaji mapato, pengo la mapato ya Sh.**4,355.1** milioni linajazwa kwa njia zifuatazo:

| HATUA | MAPATO MAPYA (Shs. Million) |
|---|---|
| i) Kuanzishwa kwa kodi ya VAT na kufuta baadhi ya kodi | 6,635.1 |
| ii) Marekebisho ya Mfumo wa Ushuru wa Forodha | 0.0 |
| iii) Marekebisho kwenye kodi ya mauzo nje | (5,780.0) |
| iv) Uuzaji nje wa chuma chakavu | 0.0 |
| v) Marekebisho ya kodi za mafuta ya petroli | 0.0 |

| | | |
|---|---|---|
| vi) | Marekebisho ya kodi za magari | 0.0 |
| vii) | Kuhamasisha soko la mitaji | 0.0 |
| viii) | Marekebisho ya ada na tozo (charges) mbali mbali zinazo-kusanywa na Wizara na Mikoa | 3,500.0 |
| ix) | Kuimarisha usimamizi katika ukusanyaji wa kodi. | 0.0 |
| | **JUMLA YA MAPATO MAPYA** | **4,355.1** |

**Sura ya Bajeti:**

93. Kutokana na maelezo ya mfumo wa bajeti yaliyotolewa hapo juu, sura ya bajeti itakuwa kama ifuatavyo:-

| **Mapato** | | | **Shs. Milioni** |
|---|---|---|---|
| **a)** | **Mapato ya Ndani** | | **699,521.0** |
| | ***i) Mapato ya kodi*** | ***632,784.7*** | |
| | ***ii) Mapato yasiyo ya kodi*** | ***62,381.2*** | |
| | ***iii) Mapato mapya*** | *4,355.1* | |
| b) | Misaada na mikopo ya nje | | **309,265.0** |
| c) | Mikopo ya Ndani | | (10,000.0) |

| | | |
|---|---|---|
| d) | Mapato kutokana na Ubinafsishaji | 9,000.0 |
| Jumla ya Mapato yote | | 1,007,786.0 |

Matumizi

| | | |
|---|---|---|
| e) | Matumizi ya kawaida | 743,321.0 |
| | *i) Wizara* | *302,232.1* |
| | *ii) Deni la Taifa* | ***209,123.0*** |
| | ***iii) Mikoa*** | ***16,411.1*** |
| | ***iv) Matumizi Maalum*** | ***111,034.1*** |
| | (a) Electricity Bills | 15,000.0 |
| | (b) Payment of Arreas | 14,469.0 |
| | (c) Road Fund | 46,072.0 |
| | (d) TRA/CMSA | 19,581.0 |
| | (e) Contingency | 15,912.1 |
| | v) Serikali za Mitaa | *104,520.7* |
| | *(a) Miji* | *20,307.1* |
| | *b) Wilaya* | *84,213.6* |
| f) | Matumizi ya Maendeleo | 264,465.0 |
| | *i) Fedha za Ndani* | *10,000.0* |
| | *ii) Fedha za Nje* | 254,465.0 |
| | **Jumla ya Matumizi yote** | **1,007,786.0** |

## Mwisho:

94. Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka 1998/99 imeandaliwa kwa kuzingatia mazingira magumu ya kiuchumi. Hali mbaya ya hewa imeleta madhara makubwa katika uchumi wetu. Ni matumaini ya Serikali kuwa mwaka 1998/99 utakuwa na nafuu katika mabadiliko ya hali ya hewa. Aidha, zipo taarifa kuwa pamoja na hali mbaya ya mvua za ELNINO, maeneo mengine nchini yamefarijika kwa kupata mazao mengi ya chakula na biashara kama vile mpunga na pamba. Neema hii itasaidia sana katika kujazia pengo la chakula na mauzo nje katika mwaka 1998/99. Hata hivyo, ili mazao haya yaweze kuleta faida inayotarajiwa kwa watanzania wote, matengenezo ya njia za usafiri na usafirishaji ni muhimu sana. Kama nilivyoeleza hapo awali, bajeti ya mwaka 1998/98 inalenga katika kutekeleza na kufanikisha kazi hiyo.

95. Mheshimiwa Spika, kwa kutambua uanzishaji wa kodi ya VAT, Serikali haikutaka

kufanya marekebisho makubwa katika kodi nyingine jambo ambalo lingeathiri sana mapato ya wananchi ambayo tayari ni madogo. Kwa upande mwingine, hatua za kufuta kodi ya mauzo nje inategemewa kuongeza kipato cha wakulima kwa kiwango fulani. Ni matumaini ya Serikali kuwa, wauzaji nje wa mazao yanayohusika na kufutiwa kodi hii hawataongeza faida yao tu bali wataongeza pia bei za wakulima.

96. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

## MWENENDO WA BIDHAA YA VIGEZO MUHIMU VYA BIASHARA YA NJE 1991 - 1997

Jedwali Na. 1

(US $ Milioni)

| Mwaka | 1991 | 1992 | 1993 | 1994 | 1995 | 1996 | 1997* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Mauzo ya Bidhaa nchi za nje.............. | 362.3 | 397 | 439.3 | 519.36 | 682.92 | 761.67 | 721.34 |
| 2. Uagizaji toka nje... | 1269.96 | 1361.97 | 1274.89 | 1309.32 | 1340.67 | 1212.63 | 1337.72 |
| 3. Urari wa Biashara ya Bidhaa............. | -907.66 | -964.97 | -835.59 | -789.96 | -667.75 | -460.96 | -616.38 |
| 4. Urari wa Biashara ya Bidhaa kama % Mauzo ya Bidhaa nchi za nje | -250.5 | -243.1 | -190.2 | -152.1 | -96.3 | -69.2 | -86.4 |
| 5. Uagizaji wa mafuta ya Petroli | 136.1 | 181.9 | 167.2 | 148.86 | 193.82 | 158.38 | 187 |
| 6. Uagizaji wa mafuta ya Petroli kama % Mauzo ya Bidhaa nchi za nje. | 37.6 | 45.8 | 38.1 | 28.7 | 28.4 | 20.8 | 25.9 |

* Matarajio

**Chanzo: Tume ya Mipango**

## MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA KAWAIDA YA SERIKALI (1992/93 - 1998/99)

Jedwali Na. 2 (Sh.Milioni)

| Mwaka | 1992/93 | 1993/94 | 1994/955 | 1995/96 | 1996/97 | 1997/98* | 1998/99** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mapato ya kawaida........ | 164110.0 | 242444.0 | 329660.0 | 448373.0 | 572030.0 | 627500.0 | 699521.0 |
| Matumizi ya Kawaida pamoja na marejesho ya mikopo(Principal)............. | 275509.0 | 340140.0 | 459564.0 | 470014.0 | 606308.0 | 711851.0 | 743321.0 |
| Matumizi ya Kawaida ukiondoa marejesho ya mikopo(Principal).............. | 240349.0 | 296221.0 | 406882.0 | 416068.0 | 553608.0 | 664551.0 | 667593.0 |
| salio la Bajeti ya Kawa-ida........................................ | -111399.0 | -97696.0 | -129904.0 | -21641.0 | -34278.0 | -84351.0 | -43800.0 |
| Salio % ya matumizi ya Kawaida | -40.4 | -28.7 | -28.3 | -4.6 | -5.7 | -11.8 | -5.9 |


* Matarajio.

** Makadirio.

Chanzo: Wizara ya fedha

Jedwali Na. 3. **MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA KAWAIDA YA SERIKALI**

(Kwa mwaka unaoishia Juni) ( Shs. milioni)




chanzo: Wizara ya Fedha

## MUHTASARI WA KIASI CHA MAZAO MUHIMU YA BIASHARA YALIYONUNULIWA
## (TANI ZA METRIKI)
## 1992/93 - 1997/98

jedwali Na. 4

| Mwaka | 1992/93 | 1993/94 | 1994/95 | 1995/96 | 1996/97 | 1997/98* |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mkonge** | 29601 | 17690 | 19459 | 22158 | 15700 | 30000 |
| Kahawa | 57367 | 34051 | 42249 | 53376 | 42441 | 38000 |
| Pamba | 307422 | 148953 | 124240 | 251171 | 252884 | 208155 |
| Tumbaku | 21953 | 25643 | 22629 | 28370 | 35379 | 51993 |
| Pareto | 2050 | 466 | 460 | 426 | 425 | 550 |
| Majani ya chai | 96950 | 102391 | 116462.8 | 97345 | 90928 | 119600 |
| Korosho | 39323 | 46598 | 63403 | 81729 | 63032 | 93173 |

***Chanzo:- KILIMO***

* Makisio

** Takwimu za mwaka k.m 1989=1988/89

### BIDHAA ZILIZOUZWA NJE 1992 - 1998
Thamani katika US$ mil, kiasi katika Tani 1000 za Metriki, Bei ya wastani katika $/Tani

Jedwali Na.5

| MWAKA | 1992 | 1993 | 1994 | 1995 | 1996 | 1997 | 1998* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **KAHAWA:** | | | | | | | |
| Thamani | 62.42 | 96.08 | 115.36 | 142.60 | 137.77 | 120.21 | 98.97 |
| Kiasi (mt) | 52.72 | 58.59 | 37.00 | 47.97 | 64.00 | 46.61 | 44.35 |
| Bei ya Wastani | 1184.00 | 1639.92 | 3117.71 | 2972.68 | 2152.66 | 2579.03 | 2231.90 |
| **PAMBA:** | | | | | | | |
| Thamani | 97.62 | 78.37 | 105.12 | 120.15 | 137.70 | 115.29 | 90.42 |
| Kiasi (mt) | 72.80 | 61.15 | 60.00 | 70.88 | 89.70 | 77.33 | 51.87 |
| Bei ya Wastani | 1341.00 | 1281.53 | 1752.02 | 1695.10 | 1535.07 | 1490.82 | 1743.18 |
| **KATANI:** | | | | | | | |
| Thamani | 1.30 | 3.33 | 5.12 | 6.31 | 4.99 | 8.57 | 6.14 |
| Kiasi (mt) | 4.11 | 4.89 | 7.20 | 11.34 | 7.90 | 13.70 | 8.33 |
| Bei ya Wastani | 317.00 | 672.83 | 711.07 | 556.44 | 631.58 | 625.30 | 847.93 |
| **CHAI:** | | | | | | | |
| Thamani | 23.63 | 30.03 | 35.52 | 23.39 | 28.32 | 29.65 | 47.40 |
| Kiasi (mt) | 20.37 | 18.75 | 21.87 | 21.60 | 26.70 | 20.40 | 25.18 |
| Bei ya Wastani | 1160.00 | 1625.54 | 1623.08 | 1081.40 | 1065.59 | 1453.51 | 1882.20 |
| **TUMBAKU:** | | | | | | | |
| Thamani | 27.93 | 17.97 | 20.58 | 27.13 | 47.01 | 12.29 | 29.53 |
| Kiasi (mt) | 13.09 | 10.82 | 15.40 | 17.08 | 24.02 | 6.25 | 14.51 |
| Bei ya Wastani | 2133.00 | 1807.94 | 1336.19 | 1588.41 | 1957.12 | 1966.82 | 2035.71 |
| **KOROSHO:** | | | | | | | |
| Thamani | 25.85 | 23.31 | 51.16 | 64.00 | 93.78 | 68.77 | 53.88 |
| Kiasi (mt) | 32.83 | 32.18 | 65.00 | 75.56 | 121.15 | 106.82 | 72.07 |
| Bei ya Wastani | 788.00 | 724.73 | 787.00 | 847.01 | 774.10 | 692.07 | 748.82 |
| Thamani Jumla Ndogo | 238.75 | 259.19 | 330.84 | 383.55 | 447.39 | 354.75 | 320.45 |
| Mafuta ya Petroli | 20.00 | 8.10 | 5.52 | 10.98 | 11.08 | 12.39 | 12.38 |
| Madini | 40.80 | 69.80 | 30.00 | 44.88 | 50.36 | 92.91 | 102.18 |
| Bidhaa za Viwanda | 115.00 | 52.00 | 77.90 | 109.25 | 110.81 | 178.13 | 120.78 |
| Nyinginezo | 75.00 | 53.80 | 70.80 | 134.26 | 142.07 | 84.30 | 74.27 |
| Thamani Jumla Ndogo | 250.80 | 183.70 | 182.52 | 299.37 | 314.33 | 363.50 | 315.57 |
| Thamani Jumla Kubwa | 495.31 | 430.89 | 519.36 | 682.92 | 761.72 | 721.36 | 642.02 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania — Makadirio

**Jedwali Na.6** **BIDHAA ZILIZOAGIZWA NJE 1992-1998**

Katika Dola Mil.(US $)

| Mwaka | 1992 | 1993 | 1994 | 1995 | 1996 | 1997 | 1998* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **BIDHAA ZA VIWANDA..............** | 700.5 | 632.9 | 656.5 | 554.2 | 501.03 | 496.32 | 559.25 |
| Usafirishaji | 339.4 | 262.3 | 242.3 | 209.65 | 202.73 | 187.39 | 252 |
| Ujenzi | 116.3 | 103.5 | 107.5 | 49.22 | 42.52 | 31.8 | 61.7 |
| Mashine | 244.8 | 267.1 | 306.7 | 295.33 | 255.78 | 277.13 | 245.55 |
| **BIDHAA ZA KATI..........................** | 333.8 | 296.2 | 290.26 | 608.96 | 530.99 | 450.36 | 389.95 |
| Mafuta ya Petroli | 181.9 | 167.2 | 148.86 | 193.82 | 158.38 | 187 | 123.13 |
| Mbolea ya chumvichumvi | 16 | 11.3 | 11.7 | 11.75 | 23.34 | 19.36 | 20.84 |
| Bidhaa zisizosindikwa | 135.9 | 117.7 | 129.7 | 403.39 | 349.27 | 284 | 245.98 |
| **BIDHAA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA......................................** | 388.3 | 312.2 | 359.5 | 377.65 | 361.81 | 351.04 | 491.5 |
| Chakula | 48.9 | 93.7 | 127.5 | 44.2 | 52.67 | 57.85 | 112.2 |
| Nyingine | 339.4 | 218.5 | 232 | 333.45 | 309.14 | 293.19 | 379.3 |
| **BIDHAA NYINGINE MBALIMBALI.................................** | 87.3 | 224.1 | 198.6 | N/A | N/A | N/A | N/A |
| Jumla | **1509.9** | **1465.4** | **1504.86** | **1540.81** | **1393.83** | **1337.72** | **1440.7** |
| T.Shs/US$ (Wastani) | 230 | 418 | 512 | 558.2 | 582.2 | 618.35 | 650 |

**Chanzo:** **Benki Kuu ya Tanzania** * **Makadirio**

Table No. 7 **TANZANIA: DEBT SERVICING (July 1997 - April 1998)**

(In T'shs. Million)


| Month | DOMESTIC | | | | | EXTERNAL | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Contractual | Interest on stocks | Treasury Bills [illegible] Amortisation | Promisory Notes | Treasury Bonds Interest and redemption | Paris Club | Multilateral | Others | Total |
| July 1997 | 571.40 | | 4,000.00 | | | 5,019.50 | 7,609.10 | | 17,200.00 |
| August 1997 | 563.70 | 1,229.60 | 5,000.00 | | | 5,200.00 | 3,390.20 | 1,816.50 | 17,200.00 |
| September 1997 | 2,240.20 | 2,106.90 | 3,121.20 | | | 3,329.70 | 3,948.90 | 2,174.30 | [illegible] |
| October 1997 | 1,800.30 | 439.70 | 1,324.60 | | | 5,277.80 | 5,017.20 | 3,350.30 | 17,139.90 |
| November 1997 | 3,300.00 | 451.44 | 2,392.20 | 200.00 | | 4,500.00 | 1,256.21 | 3,792.35 | [illegible] |
| December 1997 | 2,200.00 | 765.00 | 2,696.60 | | | 4,988.00 | 5,879.00 | 1,325.00 | [illegible] |
| January 1998 | 2,200.00 | 1,641.00 | 4,200.00 | 245.00 | | 3,534.00 | 5,548.00 | | 17,368.00 |
| February 1998 | 2,225.00 | 1,893.60 | 1,720.30 | | 5,000.00 | 4,988.20 | 3,099.90 | 93.30 | [illegible] |
| March 1998 | 2,255.00 | 1,953.80 | 2,773.90 | 1,613.40 | | 3,500.00 | 5,204.50 | | [illegible] |
| April 1998 | 2255.00 | 693.00 | 2,800.00 | | 193.60 | 5,992.10 | 5,168.20 | 424.80 | 17,526.70 |
| TOTAL | 19,610.60 | 11,162.84 | 30027.80 | 2058.40 | 5,193.60 | 46,329.30 | 46121.21 | 12976.55 | 173,472.50 |

*Note: The average total amount of debt service due for each month during this period was Shs. 60 billion whereas average total domestic revenue was Shs. 50.0 billion per month.*

**Source: Ministry of Finance**

Kiambatisho A

## MSINGI WA BAJETI UKILINGANISHWA NA UWEZO (MTshs) 1998/99




Chanzo: Wizara ya Fedha